# Mwanakijiji

## CHAGUO LA NEEMA

...Ng'ombe wa mahari



KUTOKANA NA KISA CHA KWELI

**M. M. Mwanakijiji**

**© 2012 Haki zote za kunakili zimehifadhiwa. Inaruhusiwa kusambaza simulizi hili kama lilivyo. Hairuhusiwi kutoa simulizi hili kwa namna nyingine yoyote iwe ya picha, video, filamu, maandishi kwa teknolojia iliyopo sasa au itakayokuwepo bila ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mchapishaji.**

**Kanusho:** *Simulizi hili japo limevuviwa na tukio la kweli hata hivyo ni zao la kutunga. Mfanano wowote wa matukio, majina ya watu, mahali, makampuni au nafasi ni wa kinasibu tu na baadhi ya majina yametumiwa kwa uhuru wa kisanii.*

**MCHAPISHAJI**

**Rock City Media**
**Mwanza, Tanzania**

**Email: rockcitym@gmail.com**

## SURA YA KWANZA

**2012**

Pamoja na kwamba alikuwa ameanza mwaka wa kwanza Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam Deo Tegeule alikuwa hakosi starehe kila mwisho wa juma. Alikuwa na kundi la marafiki zake wawili – Timothy Haule na Jumanne Mamba ambao pamoja walitengeneza timu ya wanaopenda kusoma pamoja na kujirusha pamoja. Wenyewe walikuwa wanajiona wajanja sana kwani licha ya kuwa walikuwa wanapasua darasani – waliitwa vipanga -walikuwa pia ni kivutio cha wasichana wengi pale chuoni na katika hilo walikuwa hawajivungi. Walisifika pale campus kati ya wanafunzi walioingia mwaka ule kwa jinsi ambavyo waliweza kubadilisha wasichana kama kubadilisha picha za kwenye facebook.

Walikuwa ni watanashati wa kupindukia. Vijana wengine wakiume walikuwa wanawaita masupa modo wa ubishoo. Hakuna wakati wowote ambapo vijana hao watatu walikuwa wamevaa varuvaru. Wote watatu walikuwa wanatoka familia maarufu nchini. Deo akiwa ni mtoto wa Jaji wa Mahakama Kuu, Tim mtoto wa Kamishna wa Operesheni wa Jeshi la Polisi na Jumanne mtoto wa Waziri wa Nchi ofisi ya Rais (Utawala Bora). Pamoja na ujiko wa uzuri na ucheshi wao walikuwa na ujiko wa nafasi za wazazi wao. Walisomeshwa kwa pesa za wazazi wao na hawakuchukua hata tone moja la mkopo toka Bodi ya Mikopo – ambayo ilikuwa haijapungukiwa kashfa za ufisadi.

Jumamosi moja Deo na wenzake waliamua kwenda kusherehekea siku kuu ya kuzaliwa kwake. Walipanga kwenda Club Bilicanas kujirusha kwani waliamini pale palikuwa na uhuru wa aina yake kujichanganya na watu wa sehemu mbalimbali. Pamoja na kuwa na uchaguzi mkubwa wa lundo la wanawake ambao angeweza kwenda kujirusha nao alikuwepo msichana mmoja tu ambaye Deo alikuwa amepanga kumwomba watoke naye kwa siku hiyo. Alishamtongoza vya kutosha tangu walipoanana kwa mara ya kwanza pale Maktaba ya Chuo Kikuu. Binti yule alikuwa akimtolea nje mara kwa mara hasa kwa vile alikuwa miaka miwili mbele ya Deo pale chuoni na haikuwa fasheni kutoka na kijana wa mwaka wa kwanza. Lakini Deo alikuwa hajui kushindwa; kwa kadiri Lina – yule msichana - alivyomtolea nje ndivyo Deo naye alivyozidi kumbembeleza na kumwimbisha kila akipata nafasi.

Asubuhi ya siku ile ya kuzaliwa Deo alibembeleza zaidi. Alimtumia ujumbe wa simu Lina.

*Hi Baby, umefikiria ombi langu?*

*We mbona king'ang'anizi hivyo; miye niache kufikiria mambo ya maana nikufikirie wewe; sifikirii.* Aliweka alama ya picha ya uso wenye huzuni.

*Acha hivyo Lina, hata kwa birthday yangu?*

*Birthday yako lini?*

*Leo*

Kimya kikapita kidogo. Deo aliamua kuandika tena.

*Hata kuniwish happy birthday hutaki?*

*I'm sorry, happy birthday*

*Mbona kavu hivyo?*

*Unataka ije na maji?*

*Naomba basi tutoke wote jioni mara hii tu Lina please?*

*Hivi wewe hukati tamaa eh?*

*Kukata tamaa ndio nini lol*

*Nikikubali safari hii utaacha kunisumbua?*

*Kabisa nitashukuru sana.*

*Wapi unaenda kusherehekea?*

*Bilicanas*

*Ok. Nitakukuta huko*

*Are you serious?*

*Niulize tena uone kama sibadili mawazo.*

*Thanks hautajuta.*

Deo na wenzake walifika mapema kidogo pale Bilicanas usiku ule; walichagua meza iliyokuwa karibu na alipokuwa DJ. Waliagiza vinywaji kidogo huku wakisubiria washirika wao wengine na wakipiga stori za hapa na pale. Deo alikuwa anamsubiria Lina tu; mawazo yake yote yalikuwa kwa binti yule.

Muda si mrefu ukumbi ulizidi kujaa watu kila kona na muziki ulizidi kuungurruma. Kulikuwa na mwimbaji Dully Sykes aliyekuwa atumbuize usiku huo. Kwa kadiri dakika zilivyozidi kwenda ndivyo Deo alivyozidi kuwa na wasiwasi. Hakutaka kuandika ujumbe kwa Lina lakini aliamua kama Lina hatotokea basi hatotoka na msichana yoyote usiku ule. Licha ya wasichana kadhaa kujichekelesha na kujilengesha Deo aliwatolea nje. Mawazo yake yote yalikuwa kwa Lina.

Mara simu yake iliyokuwa mezani ambayo alikuwa haeshi kuikodolea macho ilitetemeka na kuonesha namba ya Lina. Aliiangalia na kukuta kuna ujumbe.

*Upo wapi?*

*Niko karibu na DJ upande wa kulia*

Moyo wa Deo ulimruka ruka na nusura asimame kwa furaha. Uso wake ulipambwa na tabasamu la utulivu. *Mla mla leo, mla jana kala nini* – aliwaza. Aliangaza macho yake kuangalia upande wa mlangoni akimsubiria kumuona Lina. Dakika chache baada ya ule ujumbe wa mwisho Lina aliingia akielekea upande alikokuwa ameketi Deo. Rafiki zake walipomuona Lina walinyanyuka kuwapisha pale mezani na kwenda kwa wasichana wao ambao walikuwa wanapiga soga na wenyewe.

“Ohh beautiful!” Deo alisema akisimama.

“Hi Deo, Happy Birthday” Lina alimsalimia kwa aibu kidogo.

“Thanks Lina, duh umependeza si utani”

“Oh thanks”

“Mungu Ibariki Tanzania!!!”

“Embu toka hapa” Lina aliachia tabasamu la wivu lililoachilia meno yake yaliyong’ara vizuri na kuonesha ni binti ambaye kicheko chake kilikuwa ni tiba tosha.

Kwa kila kipimo Lina alikuwa ni msichana mzuri. Alikuwa amevaa gauni la rangi nyeusi ambalo liliishia juu kabisa kwenye mapaja lakini likimbana vizuri mviringo wa maumbile yake ya kike. Kifuani lilikuwa limejiachia wazi hadi karibu na kitovu na kugawa matiti yake likiyafunika vizuri. Gauni lile lilijimwaga kiunoni likitengeneza mkusanyiko wa marinda na kumfanya kama Jennifer Lopez alipotoka na P.Diddy miaka kadhaa nyuma na lile gauni lake la kijani lililo. Alivaa viatu virefu vya mchuchumio vya rangi nyekundu kali na hereni za rangi ya dhahabu. Alivaa pia mkufu wa rangi nyekundu uliotengenezwa kwa marumaru za aina fulani hivi. Alijipaka rangi nyekundu yam domo na uwanja mweusi ulipamba macho yake makubwa. Kwa sekunde chache Deo hakuamini kama Lina alikuwa pale kwa ajili yake. Alijaribu kuangalia nyuma ya Lina kuona kama kuna mtu mwingine labda amefuatana naye. Hakuwepo.

“Sasa si ufunge mdomo basi duh” Lina alicheka huku akivuta kiti kukaa ndipo Deo alipopata ufahamu na kujaribu kumuwahi kumsaidia kuketi.

“Yaani, yaani, duh, mambo mzima?” alizungumza kwa kubabaika kama shetani aliyefumwa akila njama ya kunyonya damu za watu.

“Pouwa sana, pole umesubiri sana eh”

“Sasa ningefanyaje ndio kupenda kwenyewe”

“Usianze mambo yako ya kupenda, utapenda wangapi?” alisema Lina kwa kejeli iliyojaa ukweli. Macho yake yakidokeza kitu ambacho kilikuwa kimefikicha lakini kisichoweza kufichika kwa muda mrefu.

“Acha hizo hapa kwako nimepata pa kupenda kiukweli”

“Embu toka huko kwanza ntakunywa nini?”

“Sema tu” Ukawa mwanzo wa mazungumzo na kuchekeshana. Walishangaa jinsi ambavyo walikuwa wanakubaliana katika mambo mengi na kufurahia kila mtu na mwenzie.

Dakika chachae baadaye walijimwaga ukumbini kucheza. Waliwasahau Tim na J-four kama wenyewe walivyomuita. Walizungumza huku wakicheza pamoja, na Lina hakuwa mnyimi kwenye kucheza; alimtikisa na kumtikisia, kijana wa watu alikuwa hoi bintaaban. Na zilipoanza kupigwa nyimbo za chombeza time hakuna kati yao aliyejivunja. Walikumbatiana na kucheza. Lina aliamua tu kuondoa uvivu siku hiyo; aliamua tu mara moja hiyo alistahili furaha. Deo aliamini kuwa kwa Lina alikuwa amefika. Hakujua ni kitu gani kilimfanya aamini hiyo lakini kama alikuwa anatafuta hazina katika maisha yake basi alijiaminisha kuwa ameipata. Muda wote aliokuwa na Lina pale hakuwaza wala kumfikiria msichana mwingine yeyote. Kitu ambacho hakikuwa kawaida yake.

Saa nane za usiku walikuwa hoi bin taaban; siyo kwa kileo cha pombe tu bali kileo cha kuchombezana na kuchokozana. Deo alimwambia watoke na kwenda hoteli ambako alikuwa tayari ameshapanga chumba. Lina hakukataa na yeye alishachoka kuwepo Bilicanas; alitaka kwenda mahali watulie na wapeane mapenzi ya ukweli, mapenzi ya nguvu, mapenzi ya kukumbuka.

Deo alikuwa anaendesha gari dogo la Toyota Camry ya rangi ya fedha. Waliondoka pale Deo akiendesha gari. Tim na mwenzake waliamua kukodi teksi kuwarudisha chuoni. Alichukua mtaa wa Mkwepu hadi ule Jamhuri alipokata kona kulia na kwenda nayo na kuvuka kuelekea mtaa wa Ohio alipokata kushoto kuelekea Bi Titi Mohammed. Walipoishika barabara ya Bi. Titi walikuwa wanaelekea Protea Hotel maeneo ya Oysterbay. Deo alikuwa na hela ya kutosha tu hasa baada ya babake kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu na Rais Kikwete.

Kama kawaida usiku ule barabarani kulikuwa na magari mengine kidogo ya watu waliokuwa wanatoka kwenye mizunguko mbalimbali na wengine wakienda kwenye kufurahia

weekend. Pamoja na magari walikuwepo na watu nao wakitembea kwa miguu wengine wakiyumba kwa ulevi. Magari mawili ya polisi yaliwapita yakiwa yamewasha vimulimuli. Kokote yalikokuwa yakikimbia hakukuwa na mema. Joto la Jiji la Dar na harufu ya chumvi walisikia wakati wanatoka tu pale ukumbini lakini ndani ya gari lile walikuwa ulimwengu mwingine kabisa. Sauti ya chini ya muziki kutoka Passion FM ilikuwa ikisikika.

Walipofika hotelini walienda moja kwa moja chumbani na walikuwa kama mbwa walioachiliwa bila kamba. Walikuwa na njaa ya mapenzi na kama ni usongo au ukame waliamua kuuondolea uvivu. Deo aliyajua mapenzi na Lina alijua majibu yake. Kabla ya kufika kitandani walijikuwa wanamaliza raundi ya kwanza sakafuni. Walipoingia kitandani ilikuwa ni usiku wa mapenzi. Walipitiwa na usingizi majira ya saa kumi na mbili za asubuhi wakiwa hoi bin taabani. Walilala kama walivyozaliwa; wamekumbatiana bila kutamani kuachiana – Lina akiwa mbele ya Deo.

Saa nne na nusu hivi za asubuhi Lina aliamka na kwenda kujimwagia maji kidogo. Aliporudi chumbani Deo alikuwa amelala chali usingizi umemnogea. Lina alichukua simu na kuagiza chakula cha asubuhi; aliambiwa kitakuwa tayari ndani ya dakika kumi na tano hivi. Hata hivyo yeye alikuwa na njaa nyingine. Lina alijikuwa akishikwa na ashki tena. Hakutaja kujivunja. Alipanda juu kitandani na kumkalia Deo huku akimteremshia mabusu motomoto. Deo alipozinduka ilibidi atoe ushirikiano huku usingizi ukiwa umembana kichizi. Raundi hiyo ya asubuhi ilipokwisha walienda bafuni wote kuoga na walipomaliza huduma ya chakula cha asubuhi ilikuwa nje mlangoni. Walikula huku wakicheka.

“Lina naomba uwe mpenzi wangu sitaki hii iwe mwisho” Deo alibembeleza

“Acha hizo bana this was fun, and that’s it we nenda kwa wanawake zako” Lina alijibu huku akimalizia kuzifunga nywele zake nyuma kwa kitambaa chenye mpira.

“Sitaki mwanamke mwingine, nakutaka wewe”

“Deo, unajua unazungumza tu huwezi kuacha tabia yako na miye sina mpango wa kukubadilisha”

“Lina, I tell you nataka niwe na wewe kwa exclusive relationship kama utakubali”

“Deo, nitakupa deal; nenda kavunje mahusiano na wasichana wako halafu urudi; uwaambie umeamua kuwa na mimi”

“Hilo tu? Mbona si gumu?” Walicheka. Lina hakuamini kama Deo anaweza kuacha wale aliowaita “wanawake zake”. Lakini moyoni alitamani iwe kweli kwani moyo wake pamoja ujanja

wake wote ulikuwa unamlipukia sana Deo. Deo alikuwa kijana mrefu, mcheshi, sura yake ya kitoto hivi lakini mchangamfu na mwenye akili sana. Sauti yake ilikuwa kama yule mwimbaji wa zamani kipofu marehemu Nico Zengekala.

Waliondoka pale hotelini kurudi chuoni. Deo alikuwa ni mwenye furaha sana kwani kuwa na Lina ilikuwa ni upgrade ya ajabu katika mahusiano yake. Ndani ya gari walikuwa wanazungumza huku mikono ya Deo ikishindwa kujizuia kutulia kwenye mapaja manono kama ya pundamilia ya Lina. Kama kawaida yake Deo alikuwa anaendesha gari kwa mwendo wa kasi kidogo na kwa siku ya Jumapili hakukuwa na magari mengi sana na hivyo alijisikia huru kwenda mwendo kasi kidogo. Waliamua kuchukua barabara ya Ally Hassan Mwinyi kuelekea Sam Nujoma.

Walipofika kona ya kwenda Rose Garden Deo alikuwa amenogewa na kuchezeana ndani ya gari na Lina ambaye alikuwa akimkataza na kumtaka aangalie barabara. Lakini ubishi wa Deo ulimfanya ashindwa kuliona lori lililokuwa limeegeshwa barabarani baada ya kuharibika. Alikuwa kwenye mwendo mkali na hakuwa na uwezo wa kulikwepa. Alipojaribu kuingia upande wa kulia kulikuwa na daladala iliyokuwa ikielekea Mwenge. Aliyumba mara ya kwanza huku akijitahidi kupunguza mwendo kabla ya kulifikia lile lori.

Aliyumba mara ya pili wakati anajaribu kufunga breki kwa nguvu kidogo lakini kwa kadiri alivyofunga breki ndivyo ambavyo alivyozidi kupoteza kushikilia usukani wa gari. Kelele za Lina akilia kwa sauti kali “mamamaaaa weeee!!! Tunakufaaaa” zilimchangaza zaidi. Ilikuwa ni ndani ya sekunde kama tano hivi kabla Deo hajaamua kuliyumbisha gari pembeni kushoto kabisa akijaribu kupita kwenye njia ya waenda kwa miguu. Lakini matairi ya gari yalikataa kurudi kwa haraka na alipoteza uthibiti wa gari na kugonga nguzo ya taa. Gari lilipinduka mara tatu kabla ya kutulia kwenye mtaro.

“Aaaaah; Aaaaah” Lina alilia huku akijaribu kujinasua kutoka kwenye kibano cha gari na mkanda wa gari aliokuwa amevaa. Hakuweza. Mkono wake wa kulia ulikuwa hauwezi kusogea. Aliuangalia kwa pembeni na kuuona ukiwa umevunjika katikati. Damu ilikuwa inamtoka kama kuku aliyechinjwa na shingo ikashikiliwa. Hakuamini kama ilikuwa ni damu yake. Maumivu yalikuwa bado hayajingia. Upande wa kulia mbavu zilimuuma vikali na kumfanya apate shida kuhema. Alijaribu kumuangalia Deo ambaye uso wake ulikuwa umejaa damu, mdomoni akitoka damu lakini bado anathema.

Sekunde chache tu baadaye alisikia watu wakijitahidi kuwanasua na king'ora cha gari la polisi kikisikika kwa mbali. Lina hakujua kama Deo alikuwa mzima au la. Na yeye mwenyewe hakujua kama alikuwa hai kwani kitu kama usingizi mzito kilikuwa kikimjia. Aliamua kutubu dhambi zake  huku akijuta uamuzi wa kwenda na Deo. Alipoteza fahamu.

DR. TEGEULE na mkewe Neema walikimbia Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) mara tu baada ya kupata taarifa za ajali. Mtoto wao mkubwa Deo alikuwa mahututi akiwa amevunjika miguu, mikono na fuvu lake likiwa limepata ufa. Walipofika pale walipokelewa na Muuguzi Mwandamizi Fatuma Kitoshi aliyekuwa anawatarajia hasa baada ya kugundua kuwa Deo ni mtoto wa Jaji wa Mahakama Kuu. Taarifa za ajali ya Deo na Lina ilisambaa kwa haraka sana hasa kupitia mitandao ya Facebook na jumbe za simu za mikononi. Ndugu na marafiki wengine wengi walikuwa nao wanaelekea pale MOI kuwaona. Deo na Lina waliwekwa kwenye vyumba viwili tofauti ambavyo havikuwa karibu karibu.

Dr. Tegeule na Neema mkewe hawakuweza kufanya lolote zaidi ya kukaa pembeni ya kitanda cha mtoto wao kwenye chumba cha wagonjwa mahututi. Walijikuta wanasali na kuombea tu kwani hali ya mtoto wao ilikuwa mbaya sana. Hakuna aliyetoka pale chumbani isipokuwa kwenda msalani. Deo alikuwa ameshafanyiwa upasuaji wa kwanza kuweza kumfanya hali yake itengemae kidogo kabla ya kuendelea na matibabu mengine. Timu ya madaktari bingwa walikuwa wanamhudumia kwa umakini mkubwa. Saa sita za usiku Deo aliingizwa kwenye chumba kingine cha upasuaji kufanyiwa upasuaji wa pili. Alikuwa amepewa madawa makali ya usingizi na yale ya kupunguza maumivu. Alikuwa amefungwa vitambaa vya dawa karibu kila inchi ya mwili wake. Wazazi wake walisubiria bila kulala. Asubuhi na mapema Deo alirudishwa tena chumbani kwake.

Wakati huduma inaendelea kwa Deo, Lina naye alikuwa anahudumiwa upande mwingine wa hospitali ile ile. Wazazi wake walipewa taarifa mchana ule wa ajali na hawakuchelewa. Walipanda ndege ya Precision jioni ile ya Jumapili wakitokea Moshi na walifika jijini Dar giza likiwa limeanza kukaza. Walienda moja kwa moja MOI kumuona binti yao kipenzi; Lina. Pacha yake na Lina alikuwa yuko njiani akitokea Mbeya ambako alikuwa anasoma taasisi ya Ufundi Mbeya. Lina licha ya kuvunjika mkono na mbavu za kulia hakuwa na madhara sana mengine. Lakini naye alitakiwa kufanyiwa upasuaji. Na alikuwa amepumzika tu huku dawa zikifanya kazi taratibu..

Jumatatu asubuhi Dr. Tegeule baada ya kuona hali ya mwanae imetulia na kuwa hakukuwa na kitu kingine cha kufanya zaidi ya kuwomba Mungu alikubaliana na mkewe waende kumwangalia yule mgonjwa mwingine na kuwajulia hali.

“Twende tukawaone na kuwapa pole wenzetu”

“Sawa baba” Neema alisema macho yake yakiwa yamevimba. Faith mdogo wake na Deo aliachwa nyumbani kupokea wageni na ndugu waliokuwa wanakuja kutoa pole za ugonjwa.

Walimuuliza Muuguzi ili awaelekeze chumba alikolazwa yule binti aliyepata ajali na mtoto wao. Kwa kweli iliwauma kuona vijana wawili wakiwa wamepata ajali na maisha yao bila ya shaka yakiwa yamebadilishwa milele.

Walipofika chumba cha yule binti waliingi ndani wakiongozwa na Muuguzi.

“Karibuni jamani” Walikaribishwa na mama yake Lina.

“Asante” waliitikia. Moyo wa Neema uliongeza mapigo kwa kasi. Dr. Tegeule alijikuta akihisi kuishiwa na pumzi.

“Mheshimiwa karibu” sauti ya baba yake na Lina ilimkaribisha Jaji Tegeule. Hakuweza kujibu mara moja.

Jaji Tegeule alijaribu kusema kitu lakini alishindwa; Neema naye alitaka kusema kitu lakini alishindwa. Na kabla hawajasema lolote Neema alishikwa na kizunguzungu cha ghafla alianguka chini na kuzimia. Badala ya kuhangaika na mgonjwa ikabidi waanze kumsaidia Neema kupata fahamu. Manesi na wasaidizi wa manesi walimtoa pale chumbani. Dr. Tegeule alikimbia mara moja kumuangalia mkewe na alipoona amepata nafuu lakini ameketi chini analia na wauguzi wanaendelea kumhudumia alirudi ndani.

“Huyu ni Dr. Tegeule” Muuguzi yule aliyewaongoza mwanzoni alianza kuwatambulisha. “Mtoto wake ndiye aliyepata ajali na Lina” alisema Muuguzi bila kutilia uzito.

“Nooo, noooo” Baba yake Lina alipaza sauti.

“Oh My God, I’m so so sorry!” alisema kwa sauti Dr. Tegeule huku akitoka ndani ya chumba. Alikuwa amejaribu kuvumilia lakini uvumilivu ulimshinda.

Walijua ilikuwa ni wakati wa mavuno walichokipanda miaka ishirini nyuma.

Na mavuno hayakuwa mazuri.

**SURA YA PILI**
**2005**

Mapenzi ya Chris na Neema yalipamba moto. Chris alijua asingeweza kuendelea kuishi Mwanza katika mazingira ya utisho hasa baada ya mvurugano na familia ya Lugwisha. Walijaribu mara kadhaa kwenda kupatanishwa nyumbani kwa Vince lakini Vince hakutaka kusikia lolote. Msimamo wa mzee Lugwisha ulikuwa ni ule ule – ni lazima Neema apatane na kakake kwanza kwani yeye ndiye mkubwa wao na uamuzi wowote atakaochukua wao wazazi watauunga mkono. Neema alijihisi kukataliwa na familia yake na kujisikia kutupwa nje ya familia yao. Lakini na yeye alikuwa amerithi kichwa ngumu kutoka kwenye familia yao – alijiambia kuwa yuko tayari kulipia gharama ya hilo kwani ameamua kuwa na mtu aliyempenda maisha yake yote.


Miezi mitatu baada ya tukio lile Chris alipata uhamisho kwenda Songea ambapo aliteuliwa kuwa Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Ruvuma. Alichoamua kufanya ni kufunga ndoa kwa DC mara baada ya kufika Ruvuma na kumchukua Neema kama mkewe halali. Upande wa familia yake hawakuwa na tatizo na Neema.na walimpokea kwa mikono miwili. Likizo zote walienda Mhonda Morogoro nyumbani kwao.

Maisha ya Songea yalikuwa mazuri kwa wote wawili. Mtoto wao wa kwanza Deo alikuwa amejaliwa akili za babake na uzuri wa mamake. Waliishi Songea kwa miaka mitano kabla ya uhamisho mwingine. Uhamisho wa kwenda Arusha kwa nafasi kama ya Songea ulikuja wakati Chris na Neema wakiwa wamepata mtoto mwingine wa kike – walimuita Faith.

Arusha walikaa kwa miaka mitano mingine kabla Chris Tegeule hajaamua kwenda masomoni Uingereza ambako alienda kupata shahada yake ya Udaktari. Familia yake ilihamishiwa Dar huku ikihudumiwa na Idara ya Mahakama. Chris aliporudi kutoka Uingereza aliamua kuacha kazi ya Uhakimu na kwenda kuanzisha kampuni yake binafsi ya uwakili ya Tegeule Advocates ambayo ilikuwa inashughulika zaidi na  kesi za mambo ya familia.

Hawakuwa na mawasiliano yoyote na familia ya Lugwisha. Hawakujua ya uzima na magonjwa. Miaka ya mwanzo walijaribu kutaka kujua lakini walitengwa na familia hiyo.

BONYEZA PICHA KUTEMBELEA UKURASA WA FACEBOOK




**SURA YA TATU**
1992

“Mmama, mmama, bhageni bhaliza” Sauti kali ya mtoto wa kiume ilipasua anga la boma la Mzee Lugwisha asubuhi iliyokuwa na jua majira ya saa tatu hivi. Alikuwa anamuita bibi yake kumwambia kuwa kulikuwa na wageni wanakuja pale nyumbani.

“We Petero bageni bahe? Dilu dilu giki?” Mama Lugwisha aliuliza akishangaa ni wageni gani asubuhi hiyo. Alikuwa amemaliza tu kutengeneza chai wakati wanamsubiri mzee Lugwisha aliyekuwa yuko bafuni anajimwagia maji. Mama Lugwisha alitoka uwanjani na kumfuata Petero alikokuwa anaelekezea kwa kidole upande wa mashariki wa boma lao lililozungushwa miti midogo midogo ambayo ilitenganisha eneo la zizi kubwa la ng’ombe na nyumba kubwa ya Mzee Lugwisha na nyumba nyingine ndogo za watoto na mchungaji wake wa ng’ombe.

“Niyo bhaliza na ng'ombe nyinge gete gete” Petero alisema tena kwa sauti akiwa amesimama kwenye boma la nyumbani pale akiangalia upande wa magharibi ambako kulikuwa na vumbi likitimka.

Kutoka umbali kidogo waliweza kuona vumbi la kundi la ng'ombe wakiswagwa kuelekea Boma la Mzee Lugwisha. Pale kijijini Njabihale kama ilivyo sehemu nyingi usukumani kundi kubwa la ng'ombe likiwa linaswagwa mapema hivyo mara nyingi ni ng'ombe wa mahali na familia huwa inakuwa imeshajiandaa kwa ugeni wa aina hiyo. Lakini siku ile pale kwa Lugwisha hakuna aliyekuwa na taarifa za mahali yoyote au hata uchumba.

Ugeni haukuja moja kwa moja nyumbani. Kama mita mia moja hivi kabla ya kufika kwenye boma vijana waliokuwa wanaswaga ng'ombe wakawazuia kwenye kundi moja kubwa. Kwa kuangalia tu kulikuwa na kama ng'ombe hamsini hivi, wanono wanono. Mapembe yao yalikuwa yanatingishika tingishika katikati ya vumbi hilo. Mara watu watatu walitoka nyuma ya kundi hilo la ng'omba na kuanza kuelekea kwenye nyumba yam zee Lugwisha. Walipofika pale nyumbani mzee Lugwisha alikuwa ameshatoka bafuni na amevaa nguo kwani mama Lugwisha alipoona ugeni kweli unakuja kwenye boma lao alimtaarifu mzee na kumharakisha kutoka bafuni.

Chris hakuwa peke yake, alikuwa na rafiki yake Clementi pamoja na mzee Josephati Bululu aliyekuwa balozi wa nyumba kumi pale kijijini. Mzee Josephati alikuwa pia ni Mwenyekiti wa Kijiji. Walikuwa wametumia muda mrefu sana kumshawishi mzee Josephati kuwapeleka kwa Mzee Lugwisha kwani yeye mwenyewe alikataa. Ilikuwa kinyume na mila na desturi za Wasukuma lakini Chris aling'ang'ania sana. Hawakujua kwanini aliamua kwenda vile tena kwa mara ya kwanza. Lakini mzee Josephati alishinda pale alipowaambia kuwa angalau basi waende wenyewe kwanza kabla ya kupeleka ng'ombe. Waende wakajitambulishe kwa mzee Lugwisha na akikubali basi ndio wawalete ng'ombe pale.

"Karibuni wageni" Mama Lugwisha aliwakaribisha kwa uchangamfu wakati walipofika kwenye geti la boma. Alikuwa amejifunga kitenge juu ya gauni zuri la maua ua.

"Mwangaluka wa mayo" Mzee Josephati alimsalimia.

"Mwangaluka baba" Mama Maria Lugwisha alijibu. Wageni walikaribishwa ndani na walipofika sebuleni mzee Lugwisha alikuwa chumbani. Walipoketi tu Mzee Lugwisha naye alitoka akiwa amevaa kinadhifu kabisa. Ilikuwa ni kawaida yake kuvaa suruali iliyopigwa pasi na shati zuri lililochomekewa. Pamoja na kwamba alikuwa anaishi kijijini mzee Lugwisha alifanya kazi wakati wa Ukoloni na miaka karibu ishirini baada ya uhuru. Alishafanya kazi kama Mwalimu maeneo ya Bukwimba, Maswa, Bariadi, Mwanza mjini na Ukerewe. Alipostaafu ndio aliamua kurudi kijijini na kuendelea kulea watoto wake na kutunza mifugo yake. Alikuwa anavaa miwani ya macho yenye fremu ya rangi nyeusi. Nywele zake zilikuwa zimejaa mvi japo uso wake

haukuonesha uzee sana. Alikuwa ni wale wazee ambao mvi ziliwaanza mapema. Walisalimiana kwa heshima zote.

“Mzee Lugwisha” alianza mzee Josephati baadaya salamu na kujuliana hali “hawa vijana bwana wamekuja kuniamsha mimi mapema na maombi ambayo niseme mapema tu niliwakatalia”. Alisema kwa kujihami na moyoni akijisikia vibaya kupita kiasi.

“Sawa wageni hawakufuzwi labda niwasikie wenyewe”

Chris alijikuta anatetemeka vidole vyake. Lakini alijua yalikuwa ni maji aliyokuwa ameyavulia nguo. Ilimpasa ayaoge.

“Mzee” Chris alianza. “Naomba unisamehe sana kama itakuwa nimekuvunjia heshima kwa namna yoyote ile” aliendelea. “Mzee mimi nakuja kuomba baraka zako kwa ajili ya kumuoa binti yako Neema”. Kauli yenyewe haikutoka ikiwa na kujiamini. Alijikuta analamba midogo yake haraka haraka huku mapigo ya moyo yakiongezeka. Hakujua wala kudhania mwitikio wa mzee Lugwisha ungekuwa nini.

Mzee Lugwisha alinyanyua kikombe cha chai na kunywa fundo moja. Alipokiweka chini alishusha pumzi vile vile. Alimwangalia Chris, kishe yule kijana mwingine halafu akamuangalia mzee Josephat. Alikuwa ni kama anawatafutia maneno ya kuwaambia lakini asiyapate kwa haraka. Aliuma midomo yake kwa nguvu kidogo na alipoiachia alichukua kikombe chake cha chai na kujipa fundo moja. Ukimya uliokuwemo mle ndani ungeweza kugandisha ile chai kuwa barafu. Alimuangalia Chris.

“Nyinyi kwenu hakuna mila?”

Chris alikuwa kimya.

“Kwamba unaweza ukaamka tu asubuhi moja na kuswaga ng’ombe kwenda kwa mtu ati unamtaka binti yake? Kweli kwenu hakuna mila?” aliuliza tena swali lile lile akiwa ameliendelea kidogo kwa hoja.

“Mzee..” Chris alitaka kusema neno lakini hakupewa nafasi hiyo.

“Mimi sina tatizo wewe kutaka kumposa binti yangu lakini hivi ndivyo mnavyofanya kwenu?” Sauti yake ilikuwa ya juu kidogo na midogo yake ikitetemeka kwa hasira. Alijaribu kunyanyua kikombe cha chai tena ili kupata fundo jingine lakini kilivyotingishika kwenye vidole vyake aliamua kukiweka chini kama ndege iliyogoma kupaa.

“Josephati kweli unawaleta hawa vijana hapa namna hii kama vile hujui mila na desturi zetu!?” Alimuuliza Mzee Josephati ambaye alikuwa amekaa akimuangalia bila kuonesha hisia zozote.

“Lugwisha hawa vijana hadi wamefanya hivi ujue wana sababu; kwanini usiwasikilize wakuambie maana na mimi niliwabana kwa hili hili” alimjibu mzee Josephati.

“Sababu gani?!” Mzee Lugwisha alifoka. “Hivi kweli kuna sababu ya kwenda nyumbani kwa mtu na kumtaka binti yake bila kufuata mila kweli?”

“Nadhani wana sababu muulize kijana akuambie”

“Haya niambie hiyo sababu ambayo imekufanya ukusanye ng’ombe kuniletea asubuhi hivi”

“Baba, Neema ni mjamzito”

“Ati nini!!!” Sauti yake ilimshtua Mama Maria Lugwisha aliyekuwa anafanya shughuli zake jikoni.

“Kuna nini tena jamani” alikuja mbio mbio kuuliza. Haikuwa kawaida kwa mwanamke wa Kisukuma kuingilia mazungumzo ya mumewe na hasa wanaume lakini Mzee Lugwisha na mkewe walikuwa ni watu waliopatana na kupendanas sana. Hawakufungwa na baadhi ya miiko na mila.

“Ati Neema ana mimba”

Cheche za hasira hazikudumu sana maana sasa iliwapasa kumsikiliza Chris vizuri. Chris alikiri kuwa mimba ni yake na alikuwa tayari kumchukua binti yao kama mkewe ili asimwaibishe.

“Sasa kwanini usimwambie kakake hadi umekuja huku?” Mzee Lugwisha swali ambalo Chris alikuwa amejiandaa nalo kulijibu.

“Baba mimi na Vince ni marafiki sana”

“Ala! Sasa kwanini yeye hajatuambia?”

“Kusema kweli mzee yeye wala hajui kuwa mimi na Neema tumekuwa pamoja”

“Oooh! Ndio sababu!” Mzee Lugwisha alijikuta anasema kwani sasa uamuzi wa huyo kijana kwenda kule ulikuwa kwenye maudhui yake kamili. “Sasa hapa ndio penye tatizo; ilikuwaje yeye hajui na binti anaishi kwake?” Lilikuwa swali ambalo halikuhitaji majibu hasa. Lakini Chris aliandaa uongo ambao aliamini ungetosha kuwatuliza wazazi.

Aliwaambia kuwa yeye na Neema walikutana kwa nasibu tu na walipoanza kutoka hakujua kama ni mdogo wake na Vince. Hadi siku moja wakiwa tayari wameanza mahusiano Neema

alitaja kuwa anaishi na kaka yake Vince Lugwisha na Chris alipomdodosa ndipo alijua kuwa ni Vince yule rafiki yake na ndipo walipoendelea na mahusiano yao kwa kificho sana. Chis alikiri kuwa ni Vince aliyemkaribisha jijini Mwanza na wazo kuwa uhusiano wake na Neema ungeweza kuvunja urafiki wao wa muda mrefu lilimuumiza zaidi na hakujua la kufanya.

Maneno yake yalikuwa mazuri, sauti yake ilidokeza ukweli wa alilokuwa akilisema. Hata hivyo simulizi lake lote hilo lilikuwa likiingia upande mmoja wa sikio la mzee Lugwisha na kutokea upande mwingine. Mzee Lugwisha alihisi amedharauliwa kupita kiasi na hakuwa tayari kuendelea kusikiliza dharau hiyo.

“Chris, nimekusikia lakini kama nilivyosema mwanzoni kwa kweli sijafurahia kabisa wewe kuja nyumbani hapa kana kwamba kwenu hakuna wazee.” Mzee Lugwisha alisema kwa sauti ya taratibu lakini iliyokuwa imejaa hasira na kero. Maneno yake aliyachagua kwa utaratibu lakini akimaanisha kila herufi ndani yake. Macho yake yalikuwa mekundu yakiiva kwa hasira. Lakini alijitahidi kujitawala.

“Kwa kweli nina kila haki ya kukasirika; lakini kwa vile umekuja kwangu na kuzungumza name hilo pekee ninakuhesabia msamaha na hasa kama kweli una nia ya kumuoa binti yangu.” Alisema na kupumzika kidogo. Chai iliyokuwa mezani imebakia kidogo kwenye kikombe ilikuwa imeshapoa kwani mvuke wake ulishaacha kutoka dakika kadhaa nyuma.

“Ninachowaomba ni kwamba muondoke mkajipange upya na mumhusishe Vince”. Alisema huku akiinuka. Wote watatu waliachwa wamepigwa na butwaa. Kabla hajatokomea chumbani Chris alipata ujasiri wa kuuliza swali ambalo kwa kweli lilihitaji jibu.

“Sasa baba vipi kuhusu hawa ng’ombe wa mahari tulioleta?”

Mzee Lugwisha alisimama kwenye kizingiti cha mlango wa chumbani. Alifikiri kwa sekunde chache na huku akitoa miwani yake aliwaangalia na kutoa jibu moja tu.

“Hawa sasa ni adhabu ya kunidharau; kwanza kumharibu binti yangu halafu kuja kuniambia kuwa umemharibu!” alisema na kuingia ndani akibamiza mlango kwa nguvu.

Chris na wapambe wake hawakuwa na jinsi isipokuwa kuinuka kuondoka huku mama Lugwisha akiwasindikiza tu. Walipotoka nje bomani mama Lugwisha alimuita mjukuu wake mkubwa Stefano ambaye alikuwa hapo pamoja na baba zake wadogo na wajukuu wengine ambao walikuwa wameitana na kukaa nje baada ya kusikia kuna ugeni umekuja. Mama Lugwisha aliwaagiza waende wakawaswage ng’ombe na kuwahesabu. Stefano alikuwa kijana wa miaka kumi na sita na alifuatana na baba yake mdogo Maiko ambaye alikuwa ni mtoto wa mwisho wa

kiume wa mzee Lugwisha. Maiko alikuwa ametoka Bunda ambako alikuwa ameanza kazi ya Upolisi.

Dakika chache baadaye vumbi lilianza kutimka pale kundi la ng'ombe karibu hamsini, wakilia na kusukumana lilipoanza kuswagwa tena kuelekea kwenye zizi la mzee Lugwisha.

VINCE ALIKUWA ofisini kwake kwenye jengo la Maktaba ya Mwanza maeneo ya Stesheni. Ofisi yake iliangalia barabarani na kumpa mwonekano mzuri wa barabara ya stesheni ambapo treni la kwenda Dar na reli ya kati lilikuwa likianzia safari zake. Chumba chake cha ofisi kilikuwa kikubwa kikiwa na meza kubwa iliyochakaa pamoja na kabati kubwa la mafaili na kabati jingine dogo lililokuwa limejaa vitabu. Kwenye meza yake kulikuwa na mafaili kadhaa pamoja na mashine ya kuchapia iliyokuwa imewekwa karatasi. Mwenyewe alikuwa ameanza kuandika hadithi lakini alikuwa ameanza mstari mmoja tu wa kwanza. Taa kubwa ndefu ilikuwa inaangaza mle ndani japo mchana ule kule ndani walikuwa hawahitaji. Maktaba yenyewe ilikuwa imejaa kundi la wanafunzi kutoka shule mbalimbali za pale Mwanza ambao wengi wao walikuwa wametoroka vipindi shuleni na wengine kuamua kujisomea tu.

Vincent Lugwisha likuwa ni Mkutubi wa Mkoa wa Mwanza akisimamia huduma ya Maktaba. Tangu akiwa shuleni alikuwa anapenda kusoma vitabu sana na haikumshangaza mtu kuwa baadaye alikuja kuwa mkuu wa Maktaba. Majira ya saa saba mchana hivi akiwa anaendelea na kazi msaidizi wake alibisha hodi.

"Veneranda nini tena?" alimuuliza binti yule aliyekuwa mrefu kumpita Vince.

"Kuna mtoto katumwa toka nyumbani anataka kukuona" Veneranda alijibu na kumuelekeza yule kijana mdogo. Alikuwa Lusubilo kijana wa jirani yake pale Nyakato ambaye kwa kweli alikuwa msaada sana pale nyumbani.

"Hujambo Lusubilo"

"Sijambo anko shikamoo"

"Marhaba, nini tena wamekutuma mchana huu"

"Anti kaniambia nije kukutaarifu kuna ugeni nyumbani"

"Ugeni gani tena mbona nilikuwa sitarajii ugeni wowote?"

“Babu Lugwisha kaja nyumbani ndio nimetumwa kuja kukupa taarifa” Lusubilo alikuwa amevaa kaptula ya khaki na shati la bluu la mikono mifupi ambalo lilionekana kumbana mwilini. Alivaa kandambili tu na miguu yake ikiwa imepigwa vumbi.

Hakuhitaji maelezo zaidi. Kusikia baba yake mzee Lugwisha kaja nyumbani kwa haraka hivyo alishtuka sana. Alikuwa na wasiwasi kuwa labda mama yake ana matatizo au kulikuwa na shida nyumbani. Haikuwa kawaida ya Mzee Lugwisha kufunga safari mwenyewe. Kama kulikuwa na jambo anahitaji ilikuwa rahisi kuagiza madereva wa mabasi au kumtuma mtu aliyekuwa anaelekea Mwanza. Lakini kuamua yeye mwenyewe kuja ilitosha kumfanya aage pale ofisini. Na kwa vile ilikuwa ni Ijumaa aliamua kuacha shughuli nyingine zote za ofisi kwa msaidizi wake na yeye mwenyewe kuondoka na Lusubilo kurudi Nyakato. Alichukua gari lake la Landrover 110 ambalo alikuwa akilitumia kama Mkurugenzi wa Huduma za Maktaba. Kushotoka kwake Lusubilo alikuwa ameketi.

Iliwachukua muda kama wa dakika arobaini hivi kutoka pale ofisini hadi kufika nyumbani Nyakato. Lusubilo alielekea nyumbani kwao mita chache tu toka kwa kina Vince. Alipofika ndani alimkuta Mzee Lugwisha amekaa kwenye kochi ambalo alikuwa analipenda sana. Alimuamkia mzee wake kwa kilugha na kuketi chini.

“Baba kwema nyumbani?” aliuliza huku moyo ukimuenda mbio.

“Nyumbani ni kwema, mama yako mzima na wengine wote wazima. Swali mwanangu ni hapa kwako kwema?”

“mmh ni kwema kwani mmesikia nini?”

“Mdogo wako yuko wapi?”

Vince aliangalia haraka haraka lakini hakumuona Neema.

“Mama Kulwa Neema yuko wapi?” alimuuliza mkewe aliyekuwa jikoni akitengeneza maakuli ya mchana.

“Aliondoka hapa asubuhi kwenda mjini huko bado hajarudi”

“Ah naona hajarudi baba” Vince alirudia jibu ambalo hata mzee Lugwisha alilisikia kutoka kwa mama Kulwa maarufu pale mtaani kama Mama Wawili.

“Sawa, kwa kweli sijafunga safari hii kwa ajili tu ya kutembea. Nimekuja mwenyewe kwaa sababu nilitaka nije kukusikia wewe mwenyewe na mipango yako na mdogo wako maana ulimtuma mwezi tu haujapita kuja nyumbani kutuaga kuwa anaenda Chuo kikuu Dar” Mzee

Lugwisha alisema huku akimuangalia mwanae kwa pembeni kidogo kama mtu anayenyemelea maneno.

“Baba Neema nadhani mambo yake yako tayari; lakini sidhani kama hilo peke yake lingekuleta haraka haraka” Vince alijibu akizungumza kwa taratibu kama asiye na uhakika wa kile alichotakiwa kusema.

“Mwanangu, mimi nyumbani nilipata ugeni siku kama tatu hivi zilizopita’

“Ugeni gani tena baba?”

“Kuna kijana amekuja kujitambulisha kwangu kuwa ni mchumba wa Neema na amekuja na kundi la ng’ombe wa posa”

“Nini!!?” kwa sauti ya mshangao Vince aling’aka.

“Alikuja na rafiki yake pamoja na mzee Josephati yule Balozi wa nyumba kumi na wakanileta hizo taarifa”

“Na huyo kijana ni nani?”

“Alisema anaitwa Chris Tegeule”

‘Chris!?”

“Ndiyo na alisema ati ni rafiki yako”

Vince alikuwa kimya; midomo na mikono yake ilikuwa ikitetemeka. Alishikwa na hasira kupita kiasi. Hakutaka kuchelewa kwa mazungumzo zaidi. Aliamua kuaga wakati ule ule na kumwambia babayake kuwa anatoka mara moja na atarudi. Babake alijaribu kumtuliza ili wazungumze zaidi na asifanye jambo kwa hamaki; Vince hakutaka kusikiliza.

“Baba, kama Chris amefanya hivi siyo tu amenitukana lakini amenidharau”

“Naelewa mwanangu, lakini tutafute namna ya kulishughulikia kwa hekima”

“Yeah ngoja nikaonane naye kwanza”

Wakati anasema maneno hayo alikuwa tayari mlangoni na ufunguo mkononi. Mzee Lugwisha alimfahamu mwanae; tangu akiwa mvulana mdogo alipenda sana kuzipiga. Alipigana kwa sababu yoyote na hata bila sababu alijikuta akitafuta ugomvi tu. Mzee Lugwisha aliinuka kwa haraka kumfuata nyuma mwanae. Vince alikuwa akihema kwa nguvu huku jasho likijijenga kwenye panda la uso wake. Alipofungua mlango wa dereva na mlango wa abiria na ukafunguliwa mzee Lugwisha hakuomba ruhusa na Vince hakutaka kuuliza. Alipotia ufunguo kwenye gari alikuwa na wazo moja tu; *Chris atanitambua.*

MAGOROFA YA NHC yalikuwa upande wa kulia ukiwa unaelekea majumba ya majaji na nyumba nyingine za serikali ambazo zilikuwa upande wa kulia kule Isamilo. Upande wa kushoto kulikuwa na magorofa ya Benki ya NBC ambayo yalikuwa yamekamilika kama miezi mitatu nyuma na watu walikuwa wameanza kuhamia. Vince alipajua nyumbani kwa Chris kwani alishafika mara kadhaa. Kitu kilichokuwa kinamuudhi na kumkera ni kwamba hakuwahi kuhisi kuwa Chris alikuwa anatembea na mdogo wake. Lakini pamoja na hilo ni uamuzi wa Chris kwenda kwa mzee Lugwisha kujitambulisha na kumruka kabisa Vince aliyekuwa pale Mwanza. Hilo ndilo lililomkera zaidi ya kitu kingine chochote. Hakutaka kuelewa sababu yoyote ile. Baba yake alijaribu kumzungumzisha ndani ya gari lakini Vince hakutaka kusikia la muuza maji wala la mbeba vyuma.

Alipofika kwenye mlango wa Chris alibisha hodi kwa nguvu; haikuwa hodi ya kawaida. Na majirani walishtuka. Alikuwa amezidi kuhema kwa nguvu. Mlango haukufunguliwa. Alibisha tena; aliweza kusikia tembea tembea mle ndani na sauti ya watu kama wanabishana. Sauti moja ilikuwa ya kike.

“Fungua mlango Chris” Mzee Lugwisha alikuwa amesimama nyuma kidogo akimuangalia mwanae.

Sauti kwa mbali ilikuwa ikilia na kumbembeleza Chris asiufungue mlango. Ilikuwa sauti ya Neema akilia kama mtoto mdogo. Chris aliamua kuzungumza kupitia kwenye mlango tu bila kuufungua.

“Vince, tafadhali bwana sitaki ugomvi”

“Kama hutaki ugomvi fungua mlango basi”

“Sasa hivi kwa kweli siwezi kufungua; labda uende kwa balozi”

“Balozi!! Wakati unamchukua dadangu ulienda kwa balozi!?” aliuliza kwa hasira huku mkono wake ukijaribu jaribu kitasa cha mlango. Pamoja na kusihi sana mlango haukufunguliwa. Wakati wanajibizana hivyo kikundi kidogo cha majirani walikuwa wamesimama wanaangalia onesho hilo la mida ya saa kumi. Wanafunzi wa shule ya msingi ya Nyakabungo na wengine waliokuwa wanatoka shuleni walisimama pembeni kuangalia vile vile. Hakuna aliyejua nini kilikuwa kinaendelea. Kwa vile Chris alikuwa ni hakimu tetesi zilianza kuwa kuwa mmoja wa watu aliokuwa amehukumiwa kifungo cha muda mrefu ametoka jela na alikuwa ameenda kulipiza kisasi.

Uvumilivu ulimshinda. Alijivuta nyuma kidogo na kwa kutumia umbile lake kubwa alitumia nguvu zake zote kuupiga kikumbo mlango. Mzee Lugwisha alichelewa kumzuia mwanae kwani alipomukona anarudi nyuma alifikiri ameamua kughairi. Kabla hajasema “Vince acha” Vince alikuwa ameshachukua kasi kama ndege iliyokuwa inajiandaa kupaa.

Hakuhitaji kupiga mara mbili kwani mara ile moja tu bawaba za mlango zikaachia. Chris hakuwa na uwezo wa kumzuia kwani mlango wenyewe ulimsukumiza nyuma na alijikuta anaanguka na kuamka ghafla. Kabla hajasimama aliona nyota zaidi ya ishirini kwani Vince hakumchelewesha alimsindikiza na ngumi ya haraka haraka iliyompata sawasawa upande wa kulia wa kichwa chake.

“Kaka samahani, kaka muache” ilikuwa sauti ya Neema. Alijaribu kuingilia kati lakini alijua hakuwa na ubavu.

“Wewe unajifanya mwanamme siyo!”

“Kaka jamani, nisamehe” alipiga kelele tena

Vince ndio alimgeukia mdogo wake. Kabla hajafungua kinywa alimzaba kibao cha nguvu. Chris alikuwa amesimama tayari na kujaribu kusimama katikati yao tena.

“Vince bro samahani bana usimpige kosa ni langu”

Vince alikuwa anathema kwa nguvu kama kifaru aliyemkosakosa mtu. Hakutaka kusema mengi; hakutaka kusema la zaidi.

“Neema chukua vitu vyako twende” halikuwa wazo, ombi, au pendekezo. Lilikuwa ni agizo ambalo lilihitai kutekelezwa bila kuhojiwa. Neema hata hivyo hakusogea hata sentimeta moja.

“Neema nimesema chukua vitu vyako twende”

“Kaka siwezi kwenda” alijibu kwa sauti ya unyonge huku miguu ikimtetemeka. Alikaa mbali kabisa na kakake.

“Ati nini? Nimesema twende unanimbia huwezi kwenda au hutaki kwenda?”

Neema hakujibu.

“Nimesema twende!”

“Vince kama hataki kwenda huwezi kumlazimisha; huyu ni binti mtu mzima” Mzee Lugwisha aliingilia kati. Na ndipo Neema alipogundua kuwa baba yake alikuwa anaangalia muda wote huo.

“Baba Shikamoo”

“Sitaki shikamoo yako; kwanini umemvunjia heshima hivi kakak?” Neema hakujibu.

“Neema mimi ndio babako, nasema twende nyumbani tutafanya utaratibu ili uweze kuendelea na masomo”

“Baba hapana; miye namtunza mtoto”

“Kwa hiyo hutaki kwenda nyumbani na hutaki kuendelea na masomo?” Mzee alikuwa anafoka sasa siyo kuongea tena. Ndoto yake ya kumsomesha binti yake ili aweze kuishi maisha mazuri na baadaye kumwoza vizuri ilitoweka.

“Baba kama nimepangiwa kusoma nitasoma” Kiburi cha Neema kilikuwa kimezidi. Hakuwa binti yule aliyelelewa kijijini.

“Vince nilikuambia mimi huyu angebakia kijijini tu; unaona sasa?” ilikuwa ni lawama iliyotokana na kukata tamaa.

“Baba nikiondoka hapa sitaki tena kusikia la Neema”

“Kama nilivyosema ni mtu mzima; kama hataki kutusikia ataenda na kufunzwa na dunia” alisema mzee Lugwisha akianza kutoka zake. Mzee Lugwisha hata hakujaribu kuzungumza na Chris; ni kana kwamba Chris hakuwepo kwenye nyumba yake mwenyewe.

Vince hakukubali kushindwa. Aliamua kupiga kama mbili hivi kumwelekea Neema na kujaribu kumshika mkono kwa nguvu kumvuta waondoke. Neema alikataa kabisa akificha mikonono yake.

“Vince embu mwache bana” Chris aliingilia kati akijaribu kumzuia Vince asijaribu kumvuta Neema. Na kabla Chris hajamgusa Vince ngumi kama nyundo ilitua kwenye bega lake la kushoto. Safari hii na yeye hakukubali. Chris alirusha ngumi mbili mfululizo ambazo zilimshtukiza Vince na kumwacha anaona nyota nyota baada ya kutua kwenye uso wake. Jino lake la kukatia upande wa kulia likalegea.

Neema alijikuta anapiga kelele na mzee Lugwisha alijaribu kuwaamulia vijana hao. Lakini ilikuwa Chris aliyeamua kuachilia na kurudi nyuma. Alikuwa anathema kama ng’ombe aliyetoka kulima. Mikono yake ikitetema kwa hasira na damu yake ikichemka kwa chuki.

“Hamna haja ya kupigana; Neema nenda na familia yako” Chris alinguruma. Ungeweza kuona mvuke wa moto ukitoka kwenye pua zake. Hasira za Kiluguru zilikuwa zimefikia kilele.

“Chris hapana, siwezi”

“Nasema Nenda!” Aliamuru tena Chris.

“Mpenzi siwezi kwenda, nagtaka niwe na wewe”

“Neema ukiamua kukaa na mimi ujue siwezi kuwa na uhusiano wowote na familia ya vichaa” Chris alisema kwa kebehi.

“Unamwita kichaa nani msenge mkubwa” Vince alikuja juu.

“Ningekuwa msenge dadako angelala na mimi” ilikuwa ni matusi ya juu kwa juu; watu wazima na akili zao walikuwa wanaropokeana hadharani. Mzee Lugwisha aliona inatosha.

“Chris twende baba; kama Neema anataka kuja atatufuata na nyumbani anapajua” Mzee Lugwisha aliona mambo yameshakuwa kimbembe; alianza kuondoka taratibu. Vince alimuangalia Chris hakuweza kumlazia. Alitamani amrukie kama paka anavyomrukia panya na kumchanachana vipande.

“Neema nakuambia tena nenda na ndugu zako; nakupenda lakini siwezi kuwa na kuishi na kuhusiana na hawa kabisa” Chris alirudia tena. Neema hakusogea hata nchi moja. Neema alishafanya uamuzi. Yeye na Chrism Chris nay eye. Hakukuwa na mtu kutoka mbinuni au ahera madukani aliyekuwa anaweza kuwatenganisha.

Vince na babake walipoondoka wao wawili walikuwa katika hali ya mshtuko na huzuni kuu kwani hawakujua wanataka kufanya nini.

Hawakujua walikuwa wameanzisha kulisukuma gurudumu la aina gani katika maisha yao.

**BONYEZA PICHA KUTEMBELEA AMAZON.COM au AMAZON.EU**




**Majeruhi wa Mapenzi (Swahili Edition)** by M M Mwanakijiji (Jun 7, 2012)
$9.99 Paperback
Order in the next **58 hours** and get it by **Monday, Nov 26**.
Eligible for **FREE** Super Saver Shipping.
**Books:** See all 2 items




**Majeruhi wa Mapenzi** by M. M. Mwanakijiji (Jun 7, 2012)
$7.99 Kindle Purchase
Borrow this book for free on Kindle
Prime members read for free Join Amazon Prime
**Books:** See all 2 items

## SURA YA NNE

1992 Mwanzoni

Kwa muda wote ambapo Neema alikuwa Jeshini mawasiliano yake na Chris yaliendelea vizuri na mapenzi yao yalidumu. Kwa siri. Chris alifanya kila awezalo kwenda kumtembelea na

alifanya yote kwa kificho bila kumpa nafasi rafiki yake Vince kujua kuwa amekuwa akitoka na mdogo wake. Siku moja kama utani aliamua kujaribisha zali.

“Vince hivi utafanya nini nikiamua kumchumbia Neema” alisema huku akijichekesha. Vince alimgeukia na kumuangalia kwa jicho ambalo halikukaribisha utani kabisa.

“Aisee acha utani! Ukitaka tukosane we fanya mchezo” ukawa mwisho wa kulileta wazo hilo. Lakini moyo wake ulikuwa umeshaamua liwalo na liwe. Hakuacha mawasiliano yake na Neema. Hata wakati wote ambao Neema alikuwa jeshini likiwa kundi la mwisho la vijana walioamaliza kidato cha sita kwenda jeshini kabla ya kufutwa kwa JKT Chris alijitahidi kwa kila hali kuhakikisha kuwa Neema hadondokei mikononi mwa afande yoyote, maana maafande wengine walikuwa na uhalali wa kila kuruta.

Baada ya kutoka Jeshini mwezi mmoja kabla ya kwenda kuanza Chuo Kikuu Vince alimchukua mdogo wake Neema kwenda kumfanyia manunuzi makubwa. Kabla ya kwenda Dar kwa treni ya reli ya Kati Neema alitakiwa kwenda kijijini kwao Magu kuwaaga wazazi na kaka zake kwa muda wa wiki mbili halafu arudi Mwanza. Aliondoka asubuhi mjini mwanza kwa basi la Nyanguge kuelekea Magu kuwaona wazazi. Pamoja na mizigo yake kaka yake alimpatia mizigo mingine mingi tu ya kupeleka kijijini. Barabara ya Mwanza hadi Magu ilikuwa ni mbovu iliyojaa vumbi nyingine. Japo umbali wa kutoka Mwanza hadi Magu si mrefu hivyo lakini ilichukua karibu siku nzima kuweza kufika Magu kutokea Mwanza.

Basi lilimteremsha kwenye kituo cha basi cha Magu na kutoka hapo alisubiri gari la Landrover la kubebea abiria kuelekea kijijini kwao Njabihale. Kila mtu alifurahi kumuona na kumshangaa kwa jinsi alivyokuwa amezidi kuonekana mdada mkubwa na muda wa jeshi ulimpa ukakamavu fulani hivi ambao hakuwa nao awali. Kaka zake wa pale kijijini walifurahi kuwa naye na marafiki zake wa shule ya msingi ambao alikuwa nao wachache walikuwa bado wako kijijini wameolewa na wengine wakiwa wameshahamia mjini Magu au Mwanza na Musoma. Waliobahatika walifika hadi jiji la Dar-es-Salaam.

Muda wote ule wa mapumziko ulikuwa ni muda wa tafakari sana. Muda wa kwenda kuanza masomo Chuo Kikuu ulikuwa unakaribia na moyoni hakujisikia kabisa kwenda. Moyo wake ulikuwa kwa Chris na siyo tu kwa Chris lakini ulikuwa unataka kuanza familia. Alikuwa anapenda kusoma zaidi lakini hakuwa na hamu ya kusoma. Alipowaaga wazazi wake Mzee Lugwisha na mkewe na ndugu zake ilikuwa ni furaha kubwa kwa familia. Alikuwa anaenda na kuwa mtoto wa kwanza katika familia yam zee Lugwisha kwenda kupata elimu ya Chuo Kikuu.

Serikali ilikuwa inagharimia elimu yake la kwake lilikuwa kwenda tu na sanduku lake na mapakacha yake mengine.

Hata hivyo aliporudi kwa kakake baada ya kutumikia JKT kwa mujibu wa sheria Neema alikuwa ameshaamua moyoni. Aliamua kutokwenda chuo. Lakini uamuzi huo alijua asingeweza kumwambia kaka yake. Sababu  ya kutokwenda chuoni ilikuwa ni Chris. Wiki moja kabla ya safari ya kwenda Dar kuanza chuo Neema alienda nyumbani kwa Chris na baada ya chakula cha mchana walikuwa bado wako mezani wanapiga gumzo wakati wakisikiliza radio iliyokuwa ikirusha kipindi cha nyimbo za dini.

“Chris miye sitaki kwenda chuo bana” Neema alisema bila kuuma maneno lakini kwa sauti ya upole. Hakutaka kumwangalia machoni Chris. Alikuwa ameyaangusha macho yake chini.

“Ah hutaki kwenda Chuo kwanini?”

Neema hakuwa na jibu la mara moja.

“Kwanini hutaki kwenda chuo Neema? Nenda bana ukimaliza tu tunafunga ndoa” Chris alisema kwa sauti kali kidogo lakini iliyoficha kubembeleza.

“Miye sitaki”

“Yaani hutaki tu; huna sababu nyingine?”

Kimya.

Alipoinua uso wake, machozi yalikuwa yameanza kutiririka kama mifereji ya maji mlimani. Alikuwa na macho makubwa na angavu ambayo yalijaa upole wa aina yake yakimtuliza kila aliyekutana nayo. Chris hakutegemea kumuona mpenzi wake anatokwa machozi. Kabla ya dakika ile hakuwahi kumuona akilia kwa uchungu. Moyo wa Chris ulimuuma na aliamka kutoka upande wa pili wa ile meza ndogo ya viti vinne waliyokuwa wamekaa. Alisogeza kiti chake karibu na Neema na kuzungusha mkono begani kwake kumbembeleza.

“Neema, nini mpenzi una mimba?”

Swali hili Neema hakutaka kulijibu. Hakutaka kukiri kile ambacho alikuwa ameshakihisi kwa miezi karibu mitatu. Siri aliyokuwa amejaribu kuificha ilikuwa inakuja kutoka. Neema alikuwa na uja uzito. Alijaribu kufungua mdomo wake lakini ulimi uligoma kutoa ushirikiano wa kutoa kauli yoyote.

“Ndiyo Chris” alijibu kwa sauti yenye alama za machozi. Macho yake yalikuwa yamelowa machozi. Alikuwa anathema kwa nguvu na feni yenye shingo ndefu iliyokuwa ikipuliza pembeni haikuweza kumzuia kutoka jasho kwenye panda la uso wake.

“Are you sure Neema” Chris aliuliza macho yakiwa yamemtoka kama aliyeletewa habari mbaya.

“Ndiyo Chris, nina mwezi wa tatu sasa sijapata siku zangu”

“Sasa kwanini hukuniambia mapema?” aliuliza katika hali ya upole uliofisha woga, furaha, huzuni na hasira katika sauti moja. Neema hakutaka kusema sana.
“Duh” ndilo neon pekee ambalo Chris aliweza kulitoa. Akili yake ilianza kumzunguka kama gurudumu la mkokoteni. Koo lilimkauka kwa dakika chache na alipojaribu kuzungumza alijikuta anashindwa. Alichukua kikombe chake cha maji kilichokuwa upande wa pili wa meza na kugida mafundo kama matatu hivi. Alishusha pumzi.

“Ok baby don’t worry”

“I’m worried Chris, kaka ataniua!”

Hapo ndipo ukweli mwingine ulipenya katika fikra za Chris; Vince alikuwa bado hajui kuwa kulikuwa na mahusiano kati yake na Neema na sasa atakuja jua na akijua urafiki wao hauwezi kuwa wa kawaida. Alijua ulikuwa ni usaliti mkubwa urafiki wao. Alitamani muda ungerudi nyuma ili amwambie kabla ya kufika walipofika. Hakukuwa na jinsi. Akili yake bado ilikuwa inazunguka na pale sebuleni alipaona padogo.

“Neema ntakuoa mpenzi”

Walikuwa wameshalizungumza hilo la ndoa na Neema alijua kweli Chris alimaanisha kuhusu kumuoa. Hata hivyo Chris alikuwa na mawazo mengine. Baada ya kumbembeleza na kumhakikisha Neema kuwa wataendelea kuwa pamoja walianza kujadiliana nini cha kufanya. Uamuzi waliofikia ulikuwa ni kuharakisha ndoa bila kumhusisha kwanza Vince. Chris aliamua wiki iliyofuatia kufunga safari kwenda Njabihale kwa mzee Lugwisha kujitambulisha. Aliamini kwa kufanya hivyo anaweza kutengeneza mazingira mazuri ya kumfikia Vince.

“Chris please don’t ever leave me” Neema alisema akiwa mikononi mwa Chris.

“I promise sitakuacha kamwe Grace” Chris aliapa akitumia jina la Grace ambalo yeye mwenyewe alilipenda badala ya kumuita Neema. Midomo yake ilikutana na ile ya Neema na cheche za mapenzi yaliyokuwa yamejaa hisia kupita kiasi ziliwaka mbele yao. Ndimi zao ziliposalimiana mikono yao ilikuwa imeanza kazi ya kufunguana nguo walizokuwa wamevaa. Hawakufanya kwa papara bali kwa utaratibu wote uliojaa heshima na mapenzi. Vidole vyenye baridi vya Neema vilipita mgongoni mwa Chris na kumsisimua.

Mlio pekee pale sebuleni ulikuwa ni wa feni ikinguruma huku ikigeuka upande upande taratibu kama twiga mvivu. Neema alianza kuvifungua vifungo vya shati la Chris lililokuwa la mikono mifupi na lenye rangi nyekungu iliyokatwa vimiraba vidogo vidogo vya rangi nyeupe. Mikono yake iliweza kuhisi mapigo ya moyo yakiongozeka ndani ya kifua kipana cha Chris. Chris alichokifanya kwanza ni kwa taratibu kuvua miwani ya Neema toka kwenye uso wake ambao bado ulikuwa umeachwa na alama za machozi yaliyokaukia mashavuni. Ndani ya sekunde chache tu walikuwa kama walivyozaliwa pale pale sebuleni.

Chris alivuta kiti chake na kukikalia.

“Njoo mpenzi”

Neema aliitikia; hisia zake na vionjo, mawazo na matamanio yake yote ya kike viliitikia. Hakukuwa na mtu mwingine kati yao, hakukuwa na hofu, hakukuwa na jambo lolote ambalo lingeweza kuwatenganisha. Walianza kupeana mapenzi tena; Neema binti wa Kisukuma alikuwa kama mcheza *wigashe; ngoma ya wigashe.*

KITABU CHA MAJERUHI WA MAPENZI SASA KINAPATIKANA MWANZA

Mwanza Book Point
Chopra Building
Kona ya Kenyetta Rd na Posta Road

Na kinatarajiwa kupatikana maduka mengine nchini

*Riwaya ya Mwaka!*

**SURA YA TANO**

Mapenzi ya Chris na Neema yalikuwa yamezama kupita kiasi. Mwezi mmoja nanusu tangu ile safari ya Dar ya mafunzo Neema na Chris waliendelea kukutana kila walipopata nafasi. Majibu ya kambi ya jeshi ambayo Neema alikuwa amepangiwa yalitoka na Neema alikuwa amepangiwa kwenda Makutupora Dodoma. Wazo la kutengana kwa muda na Chris halikuingia akilini. Neema

alikuwa anampenda yule kijana kupita kiasi. Na Chris naye alikuwa anampenda Neema kupita kiasi; walikuwa wanashindana mara kwa mara kuhusu nani alimpenda nani zaidi.

Hata hivyo kulikuwa na tatizo ambalo lilikuwa linawasumbua wote wawili sana. Chris hakuthubutu kuupeleka uso wake kwa kaka yake Neema aliyeitwa Vince. Vince na Chris walikuwa ni marafiki sana na walisoma wote huko Ilboru kabla ya Chris kwenda chuo cha uhakimu Lushoto. Chris alipojua Vince yuko Mwanza na yeye alifurahia sana. Mahusiano kati ya Chris na Neema yalianza kwa sababu ya Vince ambaye alimkaribisha Chris nyumbani kwake bila kujua kuwa alikuwa amkaribisha kumkodolea macho mdogo wake aliyekuwa akiwaandalia chakula na kusaidia pale nyumbani.

Hilo lilitokea wakati Neema akiwa kidato cha tano na akiwa amekuja likizo pale nyumbani. Chris alikuwa anajua Vince alikuwa na wadogo zake sita wote wakiwa ni wa kiume isipokuwa Neema ambaye alikuwa ni kitinda mimba. Wakati Chris ametembelea pale nyumbani Neema alikuwa hana mawazo yoyote na Chris kabisa na alimuona kwa heshima kubwa sana. Vince hakujali sana alimuambia Chris kuwa Neema alikuwa anasoma kidato cha tano kule Rugambwa. Chris hakusikia kitu kingine chochote zaidi ya jina la shule.

Hata walipoachana siku ile Chris mawazo yake yote yalikuwa kwa yule binti mdogo wa rafiki yake mpenzi. Alijitahidi kumsahau lakini hakuweza. Kila alipomfikiria mawazoni alimuona binti akileta sahani ya chakula pale sebuleni na kupiga magoti kwa heshima. Kila alipojaribu kuwawazia wanawake wengine mawazo yake yalirudishwa kwa Neema na kumuona jinsi alivyokuwa amejifunga kilemba kichwani na miwani yake utadhani mtawa mwanafunzi. Chris alijitahidi kuvumilia baada ya likizo ile na Neema aliporudi shuleni Chris uzalendo ulimshinda.

Siku moja Ijumaa aliamua kufunga safari. Aliondoka na MV. Bukoba jioni na asubuhi na mapema aliingia Bukoba ambapo alikodisha gari kumpeleka mjini ambako alifikia hotelini. Baada ya kupata kifungua kinywa na kubadilisha nguo, Chris aliondoka akiwa amevaa suruali ya jeans, raba nyeupe na shati jekundu ambalo juu yale alikuwa emevaa sweta zito la rangi nyeusi. Alikuwa amechana afro yake na yule dereva aliyemchukua toka bandarini ndiye aliyemchukua tena kumpeleka sekondari ya Rugambwa. Alipofika pale hakuchelewa kujitambulisha kuwa ni kakake Neema Lugwisha. Aliyekuwa mwalimu wa zamu hakuchelewa kutuma ujumbe kupitia mmoja wa wanafunzi aliyekuwa anapita pale ofisini kuwa Neema ana mgeni wake.

Muda wote alipokuwa akimsubiri Neema alitamani aondoke kwa ghafla. Alijua amefanya makosa makubwa na itakuwa ni aibu sana kama yule binti angekuja na kumruka. Alijaribu

kufikiria kila namna ambayo mkutano ule ungeweza kuharibika. Joto lilimpanda mwilini na nusura akose pumzi kwani kama Neema angekuja kumwambia kakake basi ingeleta mchafuko katika urafiki wao wa karibu miaka ishirini. Chris alitaka kuaga pale ofisini wakati mwalimu wa zamu akiendelea na shughuli zake. Mara mtu alibisha hodi.

“Ingia” Mwalimu aliitikia na mara moja Neema aliingia akiwa amevaa nguo za nyumbani tu. Mikono yake ilikuwa imelowa maji kwani alikuwa amekatishwa kufua nguo zake.

“Kaka Chris shikamoo”

“Marhaba mama hujambo”

Chris alishukuru miungu yote ya kwao, alipiga magoti kimoyomoyo mbele ya makaburi yote ya wahenga. Alishukuru mizimu kwa kutoabishwa.

“Wazima nyumbani?”

“Wazima kabisa nilipata tu safari ya ghafla hapa Bukoba nikasema nije kutembea kidogo hapo narudi jioni hii ya leo na Mv. Victoria” alibwabwaja huku akijuta kusema mengi.

“Mheshimiwa” alidakia mwalimu wa zamu “leo ni siku ya kwenda mjini so akipata kibali mnaweza kwenda ilimradi awe amerudi hapa wakati wa roll call ya saa kumi na mbili” alisema. “Au umekuja na kuondoka tu?”Mwalimu ambaye alikuwa kama mbeya fulani alidakia tena kabla Chris wala Neema hawajajibu.

“Ah! Kwa kweli miye nilikuwa kwa dakika chache tu si unajua wasomi wetu wako busy sana, unless kama dada mdogo hapa alitaka kwenda mjini” kwa ufundi kama mwanasheria Chris alichomoa na kuchomeka kiaina. Mpira ulikuwa umerushwa kwa Neema. Neema alikuwa amechoka kukaa shuleni mwezi mzima; alipata sababu ya kwenda kung’aa ng’aa macho kidogo.

“Mwalimu naomba kibali basi niende”. Mwalimu wa zamu hakuchelewa alichomoa makaratasi pale na kujaza jina la Neema na jina la Chris na sababu ya kwenda mjini na kumpatia nakala Neema ili ahakikishe anakuwa nao muda wote akiwa mjini akiulizwa na mtu mwingine. Neema aliaga kwa haraka kwenda kubadilisha nguo.

Dakika kama ishirini baadaye Neema alikuja akiwa amevaa sare ya Rugambwa; sketi nyekundi zenye mistari miwili ya rangi nyeupe mbele na shati jeupe alitokea. Alionekana msichana mdogo tu. Kabla hawajaondoka Chris alimkabidhi ‘vijizawadi’ kidogo vya mafuta na sukari. Neema alikimbia haraka kuvipeleka bwenini. Aliporudi uso wake ulikuwa unang’ara. Dereva alichukua barabara ya Kanazi kuelekea mjini kupitia barabara ya Buyekera na baadaye

kushika Uganda Rd. Walipofika mjini dereva aliwaacha pale hotelini ambapo Chris aliagiza chakula. Muda wote wa msafara walikuwa wako kimya wakizungumza kidogokidogo.

“Samahani kwa kukushtukiza Neema” Chris aliomba radhi mara baada ya kuletewa kifungua kinywa.

“Bila ya sahamani, sikukuuliza sasa mkutano wako umeisha maana kama umekuja leo asubuhi na leo hii hii unageuza si utakuwa umetoroka mkutanoni?” Chris ilibidi akubali tu familia ya kina Lugwisha wote vichwa.

“Kusema ukweli nilidanganya” Chris alikubali.

“Ulidanganya nini?”

“Nisamehe Neema kwa kweli nimefunga safari kuja kukuona”

“Mungu wangu!!”

“Yaani tangu siku ile nilipokuona nimekuwa nakuwaza hadi nimepitiliza”

“Yesuu!”

“Mbona unashtuka hivyo kwani we bado *mtoto?*”

“Wewe, kaka akijua?”

“Nisamehe basi sikujua utamwambia”

“Siyo mimi lakini kaka…”

“Neema, sijaja kukuomba uchumba au ndoa; nimekuja naomba tuwe marafiki tu lakini usimwambie kakako atatuua” Chris alisema kwa sauti ya kubabaika lakini ikiupenya moyo wa Neema kama kisu cha moto kwenye sabuni ya mbuni. Neema hakujua cha kufanya, hakujua aitikie vipi, lakini alikuwa na uhakika mmoja alihitaji kurudi shuleni mara moja.

“Kaka Chris samahani, kwa kweli siwezi na mimi bado niko shule. Naomba unirudishe tu shuleni” Ukimya ulifuatia kwa muda. Chris alifikiria lakini alijua kubembeleza sana pia siyo kuzuri alimradi ujumbe umetumwa.

“Sawa, basi niache nikufanyie shopping kidogo kabla sijakurudisha ok” alisema huku akijaribu kuugusa mkono wa Neema uliokuwa pale mezani. Walimaliza kula bila kuzungumza sana. Baada ya Neema kwenda msalani kidogo alipotoka waliondoka kuelekea madukani ambapo Chris alijitutumia na kumpa uhuru Neema kuchagua chochote alichokitaka. Neema hakutaka kumtia kaka wa watu hasara wala kujiingiza kwenye deni; alinunua soksi, jozi moja wa malapa pamoja na mafuta ya YU. Licha ya kuambiwa anunue chochote Neema alishukuru tu kwani alikuwa na zaidi ya mahitaji yake.

Kabla ya saa saba mchana walikuwa wamefika shuleni Rugambwa. Majengo ya matofali ya kuchoma ya sekondari ile iliyoanzishwa na Kardinali Rugambwa yalikuwa yanavutia kutoka mbali. Mapaa ya vigae ya nyumba za walimu yalifanya shule ya Rugambwa ipendeze kwa kila anayetembelea. Kulikuwa bustani za maua zilizopamba njia ya kuingilia shuleni.

“Umenisamehe lakini Neema?” Chris alimuuliza baada ya Neema kuchukua vitu vyake vyake na kusimama kuaga.

“Hujakosea Ka’Chris ni kawaida tu”

“Sasa niondoke na jibu gani umekubali urafiki wangu au umekataa?” Chris aliamua kung’ang’ania kwani hakukuwa na kosa katika kujaribu.

“Miye sijui kwa kweli Ka’Chris”

“Nikuombe ufikirie basi sawa?”

“Haya naona kengele imelia”

“Haya utafikiria au haya umesikia kengele?”

“Kwa heri kaka”

Neema alianza kuondoka taratibu.

“Hey Neema!” Chris aliita kabla Neema hajafika mbali sana.

“Bee!”

“Ntakuja tena like in a month hivi hutamind nikikutembelea tena?”

“That’s ok!”

Chris hakutaka kuharibu. Alitabasamu akimuangalia Neema akitembea taratibu na mifuko yake aliyotoka nayo mjini. Hakutaka kuangalia sana kwani moyo ulizidi kumwenda mbio. Neema alikuwa amejaliwa lile umbo la uchokozi ambalo mwanamke aliyenalo anajijua analo. Umbo ambalo binti akipita lazima shingo zigeuka; za wanaume, wanawake, wazee na watoto. Neema alikuwa na umbile hilo. Chris aliondoka kwa matumaini na moyo wa furaha.

Mwezi mmoja baadaye alipokuja kumtembelea tena Neema hakuwa mgumu sana katika mazungumzo kama ilivyokuwa mwanzo. Na huo ndio ulikuwa mwanzo; mwanzo wa penzi lililokatazwa, penzi ambalo wote wawili walijua halikutakiwa kujulikana. Ulikuwa mwanzo wa moto wa mapenzi kati ya Chris na Neema.

**SURA YA SITA**

1992

Neema alijiangalia uso wake kwa kutumia kioo alichoshika mkono wa kulia. Nywele zake zilikuwa zimesukwa kwa mafungu ya mabutu madogomadogo yaliyounganishwa kwa nyuzi nyeusi. Alikuwa amejifunga doti moja ya kanga ya rangi ya bluu na nyeusi ambayo ilinunuliwa na mamake. Upande mmoja wa kanga hiyo aliufunga kiunoni na kile kipande kingine kikipita

kifuani na kutenganisha matiti yake nay a kuyafanya yawe kama vichuguu viwili visivyo na majani.Kanga ilimzunguka shingoni ilitengeneza fundo dogo alilolifunga mara mbili. Hakuwa na kitu kingine chochote chini ya kanga hiyo isipokuwa mkufu mdogo wa rangi ya dhahabu aliokuwa amepewa zawadi na Chris Tegeule.

Alipojiangalia tena aliridhika kuwa mafuta aliyokuwa amejipaka usoni yalikuwa kwa kiwango sahihi kabisa; alichukua lipstick nyekundu na kujipaka kwenye midomo yake myembamba. Aliibana midomo kidogo baada ya kumaliza na kwa kutumia kitambaa kidogo alijifuta kingo za midomo yake. Hakuwa mtu wa mapambo sana kwani alikuwa anajijua ameumbwa mwenye sura nzuri na haiba ya kuvutia. Aliweka kioo kwenye meza ndogo iliyokuwa chumbani mwake na kuchovya kidole chake kwenye kikopo cha mafuta ya Vaseline. Ukiondoa kioo kilichokuwa karibu na dirishani, chumba chake kilikuwa ni mlundiko wa vitu vingi. Kulikuwa na kitanda kidogo, meza, kabati la nguo pamoja na maboksi ambayo kakake alikuwa ameyahifadhi pale ndani yakiwa na vitabu na vitu vingine ambavyo vilikosa nafasi sehemu nyingine pale nyumbani. Neema hata hivyo aliweza kupanga vitu vyote vizuri na kufanya chumba chake kionekane kuwa na nafasi ya kutosha tu.

Taratibu alianza kupaka mafuta miguu yake baada ya kuvuta kanga ile aliyoifunga kiunoni hadi juu kabisa ya paja lake la kulia. Miguu yake ilikuwa na makovu kidogo ya utotoni ambayo yalitokana sana na kuota moto akiwa binti mdogo. Alipomaliza mguu wa kulia alifanya vile vile kwa mguu wa kushoto. Alipomaliza miguu alichukua nguo yake ya ndani iliyokuwa kitandani na kuivaa. Alizungusha mikono yake mgongoni na kuachilia ile kanga nyingine ambayo ilikuwaa imemkaa chingoni. Kanga ikaangukia kiunoni na kumfunua kifua chake. Matiti yake yalikuwa ni ya kiwango cha kati lakini yakiwa yamechomoza kama vilima vya Kibo na Mawenzi- bila theluji.

Alichovya tena mafuta na kuanza kujipaka taratibu huku mwili wake ukipata msisimko akimfikiria Chris. Mawazo machafu yaghafla yalimuingia na kumfanya ajisikite kutetemeka kama kupigwa na baridi la ghafla. Miguu yake aliona ni dhaifu. Wimbi hilo la ashki lilimpita kwa haraka lakini likiacha nyuma upepo wake ukitetemesha kila kinyweleo cha mwili wake. Alimeza fundo la mate.

Neema alikuwa amemaliza kidato cha sita na alikuwa anasubiria kwenda Jeshini kabla ya kwenda Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Christopher Tegeule alikuwa ni hakimu katika mahakama ya Wilaya ya Mwanza. Alikuwa ni kijana wa miaka thelathini na mitano na mahakama

ya Mwanza ilikuwa ni nafasi yake ya pili baada ya kufanya kazi Morogoro kama hakimu vile vile katika mahakama ya Mwanzo ya nyumbani kwao Mhonda huko Morogoro.

Mara baada ya kumaliza kuvaa Neema aliaga pale nyumbani kwao alikokuwa anaishi na kaka yake mara baada ya kumaliza shule. Familia yao ilikuwa ikiishi maeneo ya Magu ambako baba yake alikuwa anajishughulisha na kilimo cha pamba.

“Unaenda wapi tena jioni hii Neema” ilikuwa ni sauti ya wifi yake, Mama Wawili.

“Wifi naenda kwenye kwaya kanisani leo si Jumanne” Neema alisema huku akijua kuwa alichokuwa anakienda kilikuwa ni zaidi ya kwaya. Baada ya kumaliza kidato cha sita Sekondari ya Rugambwa, Bukoba Neema aliamua kukaa kwa kakake pale huku akisubiri kutafutiwa kibarua kidogo kabla hajaondoka kwenda jeshini. Licha ya kusaidia kazi mbalimbali pale nyumbani Neema alitumia muda wa jioni kwenye shughuli za kidini hasa kuimba kwaya ya kwanza katika Kanisa la Mt. Mathias Mulumba pale Nyakato Mwanza.

“Haya mama nenda usichelewe basi uje kunisaidia kuchagua mchele” Mama Wawili alimuambia wifi yake. Mama Lugwisha alikuwa na watoto wawili mapacha wa kike na wakiume; walikuwa na umri wa mwaka mmoja na nusu. Wa kiume ambaye alikuwa wa kwanza aliitwa Joseph na wa kike aliita Joycelina.

“Sawa wifi” alisema huku akichukua kipochi chake kidogo na kukishika mkononi. Alikuwa amevaa sketi ndefu ya rangi ya damu ya mzee na blauzi ya bluu yenye mikono mifupi. Pamoja na mkufu uliokuwa shingoni mwake alichoongeza ilikuwa ni bangili kama sita mkono wake wa kushoto. Hakuwa amevaa hereni japo masikio yake yalikuwa yametogwa. Alikuwa amejipulizia manukato ya YU ambayo alikuwa anayapenda sana. Kutokana na tatizo la kuumwa kichwa mara kwa mara Neema alikuwa anavaa miwani ya macho. Alipotoka pale nyumbani kwenye nyumba za NHC hakukosa salamu na miluzi ya hapa na pale. Hakuwa na maringo, alicheka alipotaka kucheka, alitabasamu alipotaka kutabasamu lakini mawazo yake yote yalikuwa ni kwa Chris. Vumbi la Mwanza lilikuwa likimkera sana lakini hakuwa pekee katika jiji la Mwanza; wote walikuwa vumbi mtindo mmoja. Na  vumbi lilikuwa limezidi wakati ule wa kiangazi kwa sababu pia kulikuwa na kampeni za mbunge na hivyo kulikuwa na matengenezo yasiyokoma ya barabara ya Nyanguge.

Alipokaribia duka la Tarimo alimuona Chris amesimama nje ya kigari chake cha Suzuki Vitara ambavyo mahakimu wa Wilaya walikuwa wamepatiwa na serikali. Ilikuwa gari dogo la

milango miwili la rangi nyekundu ambalo nyuma yake tairi lilifunikwa na nembo ya Suzuki likining'inia.

"Hujambo mama?" Chris alimsalimia mara Neema alipomfikia. Macho yake yalimuangalia Neema kwa matamanio ya simba mwenye njaa mbele ya swala aliyepotea njia.

"Sijambo shkamoo"

"Maharaba"

"Ingia twende"

Kama aliyepigwa dafrau la kurogwa na penzi Neema aliingia kwenye ile gari upande wa abiria. Hapakuwa na watu wengi bado pale dukani ambako pia kulikuwa na baa uchwara na wachache waliokuwepo walimuangalia Chris akiondoka na 'dogodogo' mmoja. Wenye wivu walishikwa na wivu wenye kumpongeza walimpongeza kimoyomoyo. Alikuwa ameopoa si utani.

"Neema!" Chris alimuita wakati akigeuza gari mara baada ya kuingia barabara kuu kuelekea Mwanza mjini.

"Bee" alijibu kwa aibu. Hakutaka kugonganisha macho yake. Moyo ulikuwa ukimlipuka kila akisikia sauti ya Chris.

"You know I love you so much" alisema kwa kimombo lakini kwa lafudhi kali ya Kiluguru. Neema nusura acheke maana ilisikika kama *yu noo ai lavi yuu soo machi.*

"I love you too Chris" Neema alisema. Macho yao yalipogongana lile wimbi la ashki lilipita tena hadi kwenye vidole. Neema alisikia ubaridi ukipita kwenye uti wa mgongo; ubaridi uliomletea maumivu ya aina fulani ambayo tiba yake ilikuwa ni Chris. Alitisa miguu kidogo bila kupenda mwenyewe. Ili kumkoleza zaidi Chris aliweka mkono wake wa kushoto kwenye paja la Neema na kuliminya kidogo.

Haikuwachukua muda kabla ya kufika nyumbani kwa Chris maeneo ya Isamilo kwenye magorofa ya NHC ambapo alikuwa amepangiwa na serikali. Haikuwa mara ya kwanza kufika pale na pale palikuwa kama nyumbani kwake Neema. Kwani kila alipopata nafasi ya kwenda mjini alikuwa anaenda kwa Chris na majirani walishamjua kama ni mpenzi wa Chris. Wakiwa pale nyumbani walikuwa huru kama vile waliokuwa wameoana.

Ilikuwa ni wiki karibu mbili tangu waonane mara ya mwisho. Neema alipewa ujumbe na mtoto aliyetumwa nyumbani siku moja kabla kuwa Chris alikuwa amerudi toka safari ya mafunzo jijini Dar na alikuwa amepanga kumuona ile Jumanne "mahali pale pale". Neema alipewa ujumbe

na mtoto wa kike wa Tarime aliyetumwa kumwambia kuna ujumbe wake pale dukani. Hamu aliyokuwa nayo kwa wiki mbili ilikuwa si ndogo.

Walipoingia ndani tu hawakuzungumza sana kwani baada ya kusalimiana kidogo na baada ya kugusana gusana pale sebuleni walijikuwa wameamua kuhamia chumbani. Chris naye alikuwa na ukame kama wa ardhi ambayo haijawahi kunyeshewa mvua. Walipokuwa wenyewe waliamua kuondoleana hamu.

“Njoo hapa mpenzi” Chris alimuita Neema aliyekuwa amesimama mlangoni akimuangalia Chris akichojoa nguo zake taratibu akiwa amesimama karibu na kitanda kikubwa kilichokuwa na magodoro mawili. Neema alikuwa akitetemeka ndani ya mifupa yake kama mtu aliyekuwa akiogopa kilichokuwa kinamsubiri. Lakini hofu ile ilikuwa imechanganyika na tamaa iliyokithiri.

“Naogopa” alisema kwa sauti iliyolegea na akizungumza kama kwa kunong’oneza.

“Unaogopa nini mpenzi, njoo bana”

Neema aliinua bega la kulia juu kuonesha kukataa. Hamu iliwazidia wote wawili.

“Jamani mpenzi, nimekumiss sana mwenzio, njoo basi darling” Chris kama mtumwa akiomba uhuru wake alibembeleza kwa sauti nzito ambayo ilizidi kumpagawisha Neema.

“Sitaki”

Chris aliinuka kama alivyozaliwa. Neema moyo ulimlipuka na miguu yake ikapigwa ganzi. Hakusogea hata nchi moja. Hakutaka kukimbia. Alikuwa tayari kwa lolote. Chris alimpofikia na kumgusa ngozi yake wimbi la tatu la ashki lilimpitia na dunia nzima kwake haikuwepo tena. Alijiachilia mikononi mwa Chris ambaye kama Zamoyoni Mogela yule mchezaji machachari wa Simba hakufanya ajizi. Taratibu Chris alianza utundu wake, utundu ambao aliupatia mafunzo jandoni. Neema alikuwa kama kipepeo mbele ya kinyonga.

“Nibusu basi mpenzi” Chris alibembeleza huku mwili wake ukimalizia kuchojoa chembe zote za nguo mwilini mwa Neema.

“Sitakiii, naogopaaa”

Chris aliamua kujifanyia vitu vyake kama aliyepewa leseni ya mapenzi. Walipojitupa kitandani ilikuwa ni fainali ya mapenzi.

**MWISHO**

Kama umesoma kitabu cha Majeruhi wa Mapenzi na unapenda kusoma zaidi hadithi hizi za Mwanakijiji na ungependa hadithi zake nyingine za huko nyuma tuandikie:

rockcitym@gmail.com

au mwandikie M. M. Mwanakijiji
klhnews@gmail.com